



APHFTA
Tanzania Private Health Sector
www.aphfta.org



P.O. BOX 13234, Dar es Salaam, Tanzania
TEL/FAX: +255 22 2120118
E-mail: info@aphfta.org

27 FEBRUARI 2024

TAARIFA KWA UMMA

YAH: TAARIFA YA PAMOJA YA VYAMA VYA WATOA HUDUMA BINAFISI ZA AFYA KUHUSU KITITA KIPYA CHA NHIF CHA BEI ZA HUDUMA ZA AFYA

Vyama vya Watoa Huduma Binafisi za Afya nchini, yaani 'Association of Private Health Facilities in Tanzania (APHFTA)', 'Christian Social Service Commission (CSSC)' na BAKWATA tunapenda kuutaarifi umma kuwa mazungumzo yaliyokuwa yakifanyika baina yetu na Wizara ya Afya kwa kupitia Kamati iliyoteuliwa na Waziri wa Afya, yameshindwa kupata muafaka kuhusu Kitita Kipy Cha NHIF Cha Bei za Huduma za Afya.

Kama Kitita kipy Cha NHIF Cha Bei za Huduma ya Afya kilichopendekezwa na Kamati teule ya Waziri kitatangazwa kuanza kutumika, itakuwa kinyume na mapendekezo ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kumalizwa kwa tatizo hili kwa maridhiano. Hivyo basi, tunautangazia umma kuwa Vituo Binafisi vya Afya vitashindwa kutoa huduma kwa wanachama wa Mfuko wa Bima ya Afya kwa kutumia Kitita Kisichokubalika kwetu.

Ili kuepuka usumbufu, wanachama wa NHIF wanaombwa kuwasiliana na Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) ili kujua namna watakavyoweza kupata huduma hizo.

APHFTA, CSSC NA BAKWATA

/
Dr Egina Makwabe
MWENYEKITI WA APHFTA.